


*Timu ya washirika wa Tujenge Nyumba ya Mungu ikiwa imewasili Wilayani **Nachingwea** kwa ajili ya kazi ya kubaini maeneo ya ujenzi wa makanisa tarehe 07/07/2023; Kulia kwao ni Mchungaji Zakaria wa EAGT Mpiruka akiwapokea. Hii ilikuwa ni safari ya kwanza ya huduma hii baaada ya kusimikwa rasmi 12/03/2023. Kushoto ni Mr & Mrs Mushi na katikati ni Mr & Mrs Mbogo.*

Pia, watu wakishiriki maombi ya kufunga yanayoitishwa mara kwa mara na viongozi kwa ajili ya safari pamoja na kuombea huduma kwa ujumla. Washirika wanaokwenda kubaini maeneo ya ujenzi nao wamekuwa wakijitoa kwa jinsi ya tofauti sana. Wao hujitoa kwa fedha zao kwa ajili ya kujikimu safarini pamoja na kuacha usingizi wao siku ya safari maana safari huwa inaanza saa 8 au 9 usiku hapa Dar es salaam. Mara nyingi safari hii huwa inahitimishwa usiku na ndipo watu hawa huwa angalau wanapata nafasi ya kupata chakula. Siku nzima kiasi kikubwa huwa hawali chakula kutokana na ufinyu wa muda maana wanakuwa wanazunguka huko vijijini mchana kutwa achilia mbali wanatakiwa kuondoka tena mapema alfajiri kwa ajili ya kuendelea na ziara ama kurudi Dar es salaam.